# RIZIKI

Machi/2024 - Mei/2024



## YESU UHAI WETU

TOLEO LA I/2024

somabiblia

RIZIKI

S.L.P. 2696, Arusha
0759 544 917
Barua pepe:
editor.somabiblia@gmail.com

**Kamati ya Riziki:**
James Sabuni (mhariri)
Mch. Anza Amen Lema
Mch. Philip Bach-Svendsen
Cathbert Msemo
Mary Bura
Magreth Mushi
Mch. Gervas Meitamei
Luhekelo Sanga

**Waandishi walioshiriki:**
Mch. Gideon Mumo
Christian

**Layout:**
Cathbert Msemo

**Jalada:**
Cathbert Msemo

ISSN 2683 - 6491

Nakala: 5000

**Usambazaji:**

**SOMA BIBLIA**

S.L.P. 2696, Arusha
S.L.P. 12772, Dar es Salaam
S.L.P. 1088, Iringa
S.L.P. 6097, Mwanza
S.L.P. 1062, Mbeya
S.L.P. 4231, Dodoma

www.somabiblia.or.tz

Neno la Injili kwa rika zote Tanzania!

**Imechapwa na:**
*Imaging Smart - Dar es Salaam*

# Aliye na Yesu anao uzima

Kulikuwa na babu mmoja ambaye alijulikana kwa hekima, busara na maarifa mengi. Wengi walimjia ili kupata maneno ya hekima, ushauri na hata upatanisho.

Mjukuu wake mmoja aliamua kumjaribu ili aone kweli ana hekima, maarifa, ujuzi na busara kama wanavyomwona wengi. Hivyo alichukua kipepeo kiganjani mwake akisema, ”Nitakwenda kwa babu na huyu kipepeo, kisha nitafunga kiganja changu. Nitamwuliza babu, ‘Kipepeo huyu yuko hai au amekufa?’ Akisema yuko hai, nitamminya na kidole changu na kumwua, kisha nitamwambia, ‘Babu umekosa’. Akisema kipepeo amekufa, nitamwachia na kumwambia babu, ‘Umekosa, kipepeo yuko hai’.”

Mjukuu alipoenda kwa babu yake na kumwuliza kama kipepeo yuko hai au amekufa, babu alimtazama usoni kwa tabasamu na kumwambia, ”Mjukuu wangu, maisha ya kipepeo huyu yako mikononi mwako! Ukitaka aishi ataishi, na ukitaka afe atakufa.”

Mada kuu katika toleo hili la kwanza la Riziki 2024 ni *Yesu Uhai Wetu*. Kama vile uhai wa kipepeo ulivyokuwa mikononi mwa mjukuu, ndivyo tunavyokumbushana kuwa uhai wetu uko mikononi mwa Yesu. Aliye na Yesu anao uzima; ambaye hana Yesu, hana huo uzima.

Makala nyingine inahusu watu ambao walipewa sharti la kumtazama nyoka wa shaba ili wapone. Ujumbe wake ni huohuo: Waliotii walipona, na waliopuuza walikufa.

*Siku zetu duniani ni kama kivuli, wala taraji ya kukaa hapana* (1 Nya 29:15). Lakini tumshukuru Mungu kwamba wote waliozaliwa mara ya pili wamepata tumaini lenye uzima kwa kufufuka kwake Yesu Kristo (1 Pet 1:3).

*James Sabuni*

## Yaliyomo:

Uk. 3-5: Yesu uhai wetu
Uk. 6-7: Musa na nyoka ya shaba
Uk. 8-9: Yesu Mfufuka - sababu ya kutoweka kwa mashaka
Uk. 10-11: Uamuzi wangu muhimu na wa busara sanaa
Uk. 12-15: Kuna maisha baada ya haya!





# Yesu uhai wetu

Katika matumizi ya kawaida ya neno, “uhai” ni hali ya kuendelea kuishi, au maisha. Katika mazingira tuliyozoea, kuna vitu vinavyowezesha maisha hayo na kuwapa watu kuishi. Vitu hivyo ni maji, chakula na hewa. Kutokana na mantiki hiyo ni rahisi kusikia watu wakisema maji ni uhai. Maji, chakula na hewa, siyo tu ni vitu muhimu, bali ni vya lazima kwa maisha ya wanadamu. Pasipo vitu hivyo, hatuwezi kuishi.

### Yesu ana umuhimu gani?

Biblia inamtambulisha Yesu kama uhai wetu (Kol 3:4). Yeye mwenyewe anasema, “*Mimi ni chakula cha uzima*” (Yn 6:48-58). Hivyo imewekwa wazi umuhimu wa Yesu katika maisha yetu.

Wayahudi wakiwa kwenye safari yao jangwani, Mungu aliwatunza kwa chakula kiitwacho *mana*. Ingawa ilitoka mbinguni, mana ilikuwa chakula cha duniani. Isipoliwa haikudumu bali kuharibika, na watu walioila walikufa.

Yesu akijilinganisha na chakula hicho cha mana, anasema katika mst.51 kwamba ndiye chakula cha kweli. Ameshuka kutoka mbinguni, na chakula anachotoa ni cha uzima, hakiharibiki, bali hukaa milele. Mtu akila hatakufa bali atakuwa hai milele.

### Yesu ni nani?

Mnamo karne ya tatu, kanisa liliingia katika mjadala mkubwa kuhusu swali hili, kwani lilikuwa katika hatari ya kugawanyika kutokana na mitazamo miwili tofauti kuhusu Yesu. Mtazamo wa upande mmoja ulikaza kuwa Yesu ni Mungu kweli na mwanadamu kweli, wakati mtazamo wa upande pili ulikaza kuwa Yesu ni mwanadamu tu, na mwenye hadhi ya juu kuliko wanadamu wengine.

Kwa kufuata Biblia, Kanisa liliamua kukiri kuwa Yesu amekuwa ni Mungu kweli na mwanadamu kweli tangu kufanyika mwili katika tumbo la bikira Mariamu.

Yesu ana asili mbili, uungu na ubinadamu. Asili hizi ziliungana Mwana wa Mungu alipofanyika mwili katika tumbo la bikira Mariamu. Kabla ya hapo alikuwa na asili moja tu, ndiyo ile ya kiungu. Asili hizi hazigawanyiki wala hazichanganyiki, bali zinadumu hivyo milele katika nafsi moja ya Yesu.

Hivyo Yesu akawa Mwokozi wetu. Yeye pekee ana uwezo wa kuokoa. Kwa kuwa ni *Mungu* kuna uzima ndani yake ambao ni nuru ya watu (Yn 1:4). Kwa kuwa ni *mwanadamu*, aliweza kuutoa uhai wake kwa ajili yetu, akawa ndiye uhai wetu. Kama Imanueli, Mungu pamoja nasi, siyo tu anatuonyesha aina ya mtu ambaye anampendeza Mungu, anatuwezesha pia kumpendeza Mungu kwa kutuita tumfuate kwa njia ya kubatizwa na kumwamini.

### Yesu anakuwa uhai wetu namna gani?

Swali hili laweza kutusaidia kuelewa nafasi ya Yesu katika maisha yetu.

Kinyume cha uhai ni mauti. Mwanadamu amepatikana na mauti kwa sababu ya dhambi (Rum 5:12).

Sasa imeandikwa hivi katika Wakolosai 3:3-4, "*Mlikufa na **uhai** wenu umefichwa pamoja na Kristo Yesu. Kristo atakapofunuliwa, aliye **uhai** wetu, ndipo na ninyi mtafunuliwa pamoja naye katika utukufu*."

Tutafakari neno hili kwa kina. Paulo anaposema tulikufa, anamaanisha maisha yale tuliyokuwa nayo kabla hatujamwamini Yesu, yale ya dhambi. Tuliyafia kwa njia ya kuunganishwa na Yesu katika kifo chake. Yesu alijitolea kwenda msalabani ili atukoe. Aliifia dhambi na kutupatia uhai mpya. Uhai huo unapatikana katika kufufuka kwa Yesu, nao ni uzima wa milele kwa sababu sasa anamwishia Mungu akiwa ameketi mkono wa kuume wa Mungu (Kol 3:1).

Tukibaki katika maisha ya zamani, hatuwezi kuwa viumbe vipya na wala maisha yetu hayo hayawezi kutengenezwa hata yawe mapya. Basi, twapataje uhai huo udumuo milele?

Tunaposoma Warumi 6:3-4, tunakutana na ujumbe wa ubatizo na maisha mapya. Paulo anaeleza vizuri kuwa sisi tuliobatizwa katika jina la Kristo Yesu, tumebatizwa katika mauti yake. Tena kwa njia ya ubatizo tulizikwa pamoja naye katika mauti yake ili, kama vile Mungu alivyomfufua katika wafu, tupate na sisi kuishi maisha mapya kwa kumwamini Yesu. "*Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama yamekuwa mapya*" (2 Kor 5:17).

### Uhai wetu uko wapi?

Ukristo, maana yake ni kuwa na uhai wa Kristo. Huenda tunafikiri juu ya uhai huo mpya kama nguvu iliyo ndani yetu ya kuishi na kushinda mauti, lakini angalia



Mtume Paulo anavyosema: Sasa hivi uhai wetu *umefichwa* pamoja na Kristo *katika Mungu*, na hapo utatunzwa vizuri hadi Yesu atakapofunuliwa siku ya mwisho wa dunia hii (ling. 1 Pet 1:3-7).

Maana yake, uhai wetu mpya sasa hivi hauonekani wazi ndani mwetu. Maisha ya zamani yenye dhambi zake bado hayajaondolewa kabisa, isipokuwa dhambi haitutawali tena. Katika Wagalatia 3:26-27 Paulo anawakumbusha Wakristo wa Galatia utambulisho wao mpya tangu walipoweka imani yao kwa Kristo Yesu. Kubatizwa ndani ya Kristo, maana yake ni yeye kuwa mtawala wa maisha yetu na sisi kumkiri kwa imani kama uhai wetu.

Tunapaswa kuelewa kwamba hali ya kuwa upya haiwezekani pasipo msaada wa Roho wa Bwana. 1 Wakorintho 12:13 inasema vizuri kuwa "*katika Roho mmoja sisi sote tulibatizwa kuwa mwili mmoja*", na mwili huu ni mwili wa Kristo. Roho Mtakatifu ndiye anayetuunganisha kwa Kristo Yesu katika ubatizo na kuendelea kutilia nguvu imani yetu akitukumbusha neno la Kristo na kutusukuma kutafuta yaliyo juu Kristo aliko (Kol 3:1).

### Nguvu ya kuwa ndani ya Kristo

Maana ya maisha mapya ni kujitambulisha pamoja na Kristo na kuvutwa kuacha maisha ya zamani ya dhambi. Tukimkiri





Yesu kama uhai wetu, tunawezeshwa hata kujikana wenyewe na kujitwika msalaba ule anaotuwekea tunapomfuata. Haya ndiyo maisha mapya ndani ya Kristo wakati wote tukiendelea kuwa hapa duniani (Mk 8:34; Lk 9:23).

Hatuwezi kuacha dhambi kirahisi. Kuondoa dhambi kunahitaji gharama au fidia. Tunawekwa huru mbali na dhambi tunapopokea kwa imani kwamba hasira zote alizokuwa nazo Mungu kuhusu dhambi zilimwangukia Yesu Kristo. Yesu aliangikwa msalabani badala yetu. Yeye asiye na dhambi aliadhibiwa badala yetu sisi wenye dhambi. Huu ni upendo mkubwa.

Kumbuka neno alilolisema Yesu msalabani: "*Imekwisha*" (Yn 19:30). Nini kilikwisha? Siyo tu maisha yake Yesu hapa duniani, bali kilichokwisha ni *mpango wake wa kuukomboa* kutoka kwa ulimwengu huu ulioanguka. Yesu akisema imekwisha anasisitiza jinsi alivyofanikiwa kutulipia kwa ukamilifu kila tendo la uasi wa zamani, wa sasa na wa baadaye. Kwa hatua hii dhambi na mauti haina nguvu tena kwao wanaoipokea habari hii njema kwa imani.

### Muunganiko maradufu

Kuwa "katika Kristo", maana yake ni kukubali kwa imani sadaka ya damu yake Yesu alipotoa uhai wake kuwa malipo halali na ya kutosha kwa dhambi zetu. Hatuwezi kwenda mbele ya Mungu Mtakatifu pasipo kufichwa katika haki ya Kristo. Kuwa ndani ya Kristo, maana yake ni kuwa Mungu haoni tena udhaifu wetu, anaona haki ya mwanawe pekee (Efe 2:13; Ebr 8:12). Ni katika Kristo tu uhusiano wetu na Mungu hurejeshwa na uzima wetu wa kudumu unatekelezwa (Yn 3:16-18, 20:31).

Hali hii nzima hutufanya tuwe na uhusiano mzuri na Mungu wetu. Njia pekee ya kutufanya wana wa Mungu ni kumpokea Kristo katika maisha yetu (Yn 1:12). Hapo Roho Mtakatifu anatuunganisha na Bwana wetu mpya kwa namna maradufu. Siyo tu kwamba tumo ndani ya Kristo, hata Yesu anaingia ndani yetu. Anafanyika kuwa uhai wetu mpya.

### Siri ya Mungu

Mwunganyiko huo wa sisi kuwa ndani ya Kristo na yeye kuwa ndani yetu ni siri ya Mungu. Paulo anawaambia Wakristo wa Kolosai kwamba Yesu kuwa uhai wao "*ni Kristu ndani yenu, tumaini la utukufu*" (Kol 1:27).

Hii ni siri iliyofunuliwa tayari kwa watakatifu wa Mungu, yaani wote wanaoishi na Yesu. Kila siku wanafanya uzoefu wa uhai walio nao Kristo akikaa ndani yao.

Hata hivyo bado ni siri. Uzoefu wao ni *wa imani*, kwa sababu Kristo, uhai wetu, bado hajafunuliwa kwa utukufu. Ameketi mbinguni mkono wa kuume wa Mungu akingojea kufunuliwa kwake siku ya mwisho.

Hapo itafunuliwa kikamilifu kwamba Yesu yuko hai naye ni uhai wetu, sisi sote tunaomwamini. Tutamwona kwa macho kama alivyo, na hapohapo tutafanana naye. Mwili wetu wa unyonge utapata kufanana na mwili wake wa utukufu (Flp 3:21), nasi tutaishi naye milele katika utukufu huo.

*Mch. Gervas Meitamei*

# Musa na nyoka ya shaba

Siku zote wokovu ni mpango wa Mungu. Mwanadamu hahusiki hata kidogo. Wana wa Israeli walipomlilia Mungu awaokoe kutoka katika utumwa wa Misri, ni Mungu aliyepanga jinsi atakavyowaokoa. Na baada ya kuwanasua kutoka katika ukatili wa Farao, Mungu, na wala sio wao, alichagua njia atakayowapitisha ili kuwafikisha katika nchi aliyowaahidia.

Wana wa Israeli hawakuwa na utulivu. Kwa hiyo waliwanung´unikia Musa na Mungu kuhusu maji, chakula na safari ya kuchosha (Hes 21). Ili kuwaadhibu kwa kunung'unika, Mungu aliwatuma nyoka wa sumu kambini, na wengi walioumwa walikufa.

> "Sisi je, tutapataje kupona tusipojali wokovu mkuu namna hii?" (Ebr 2:3)

Punde tu baada ya kutambua kwamba nyoka hawa walikuwa ni adhabu ya uasi wao, wana wa Israeli walimwomba Musa awaombee kwa Mungu awaondolee wale nyoka wa sumu (Hes 21:7). Lakini angalia, hawakuomba Mungu awaokoe tu, bali walimwelekeza Mungu atakavyowaokoa: "*Atuondolee nyoka hawa*"! Walitaka suluhisho la haraka, na kwa njia yao.

### "*Njia zenu ni njia zangu*"

Hivyo sivyo Mungu wetu anavyofanya kazi. Badala ya kuwaondoa nyoka wa sumu, Mungu alimwagiza Musa, "*Jifanyie nyoka ya shaba, ukaiweke juu ya mti, na itakuwa kila mtu aliyeumwa, aitazamapo ataishi*" (Hes 21:8).

Mungu hakuwaondoa wala kuwazuia nyoka wa sumu kuwauma. Badala yake, na sawa na agizo la Mungu, Musa aliifanya nyoka ya shaba na kuiweka juu ya mti katikati ya kambi. Maana yake, ingawa nyoka wa sumu hawakuondolewa, tiba ya kila aliyeumwa ilikuwa rahisi na karibu sana: "Tazama nyoka wa shaba utaishi!"

Nyoka wa shaba aliwekwa juu ya mti mahali ambapo kila mtu kwenye kambi aliweza kufanya nini? Siyo kumtafuta, kwenda chini ya mti au kutafuta kibali kutoka kwa Musa. La hasha! Walichohitaji ni kugeuka, kuinua macho na kumtazama nyoka wakiamini ahadi ya Mungu, na kupata uponyaji bila malipo. Hivyo tu!

Lakini sio wote walioamini na kuitikia ujumbe na mwito wa Musa. Sio wote waliokubali njia ya Mungu ya wokovu. Sio wote waliopona. Kuna waliogeukia tiba zao za kiasili, lakini wakafa. Kuna walioendelea kukaza misimamo kwamba Mungu angewaondoa nyoka wa sumu, lakini walikufa pia. Waliosubiri Mungu abadilishe njia yake ya wokovu walikufa. Hazikuwafaa sadaka, kafara au hata maombi ya kufunga. Hakukuwa na njia mbadala ya wokovu. Tiba ya sumu ya nyoka ilibaki moja tu: "Tazama utaishi!"

### "*Yaliandikwa ili kutufundisha*"

Hii leo, takribani miaka 3500 tangu Musa alipomwinua nyoka wa shaba jangwani, tunayo hali ya kutisha kupita ile ya nyoka wa sumu jangwani. Tumeumwa na nyoka aitwaye *dhambi* ambaye matokeo





ya sumu yake ni mauti (Mwa 1:27; Rum 5:12, 6:23). Siyo mauti ya mwili tu, lakini mauti ya kutengwa na Mungu milele kwenye adhabu ya moto wa milele (Mt 25:14; Ufu 21:8).

Ila, kuna Habari Njema kwetu sisi pia. Kwani kama vile Musa alivyomwinua nyoka wa shaba, ili kuleta wokovu kwao walioumwa na nyoka wa sumu, wakati ulipotimia wa kusudi la Mungu (Mwa 3:15), Yesu Kristo aliinuliwa msalabani ili kila amtazamaye kwa kumwamini apone mauti ya milele iletwayo na dhambi. Huu ndio uzima wa milele tuupatao kwa kumwangalia Yesu Kristo, Mwokozi atuokoaye kutoka kwenye adhabu ya dhambi (Yn 3:14-16, 36).

Na kama kuangalia nyoka wa shaba kulivyokuwa njia pekee ya kuwaponya walioumwa na nyoka wa sumu, Mungu amemwinua Yesu Kristo kuwa njia pekee ya kutuokoa na ghadhabu ya Mungu na mauti ya milele. Biblia inasema wazi kwamba, "*hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo*" (Mdo 4:12).



### "*Mimi ndimi njia*"

Ni kweli, kuna njia nyingi za kidini. Kisha watu wana uhuru wa kuchagua njia watakayoiendea. Lakini Yesu ndiye njia pekee ya kuingia uzimani (Yn 14:6). Basi, ni chaguo la kila mtu kumwangalia Yesu na kupata msamaha wa dhambi na wokovu, au kutomwangalia na kusubiri adhabu ya Mungu (Kum 30:19; Yn 3:36).

Tusitumie utashi wetu vibaya! Kila uchaguzi una matokeo yake. Matokeo mema au matokeo mabaya. Walioumwa na nyoka wakati wa Musa walikuwa na uhuru wa kuangalia nyoka wa shaba na kupona au kutoangalia na kufa. Nasi tuna uhuru wa kumtazama Yesu na kupata uzima au kumkataa Yesu na kupata adhabu ya milele. Uamuzi ni wa mtu binafsi. Ila Biblia inatoa tahadhari, "*Sisi je, tutapataje kupona tusipojali wokovu mkuu namna hii?*" (Ebr 2:3). Wokovu wetu u katika kumwamini Yesu (Yn 3:16). Yesu Kristo ndiye Uzima wetu.

*Mch. Gideon Mumo*

# Yesu Mfufuka - sababu ya kutoweka kwa mashaka

*Mchango kwa maandalizi ya kuhubiri juu ya Yohana 20:24-29*

Lazima kuamini. Kama ukiona shaka umepoteza kila kitu. Likatae katakata! Amini tu. Endelea kutamka kwa uhakika, Kwa jina la Yesu naamini na kupokea!

Jinsi hii tunatafuta mara nyingi kuwa na hakika juu ya imani na hata kumhakikisha Mungu tunayemwomba kwamba hatuna wasiwasi. Lakini je, tunasaidiana kweli kwa namna hiyo? Kwa nini tunaona haja ya kutamka uhakika wetu? Je, ni kwa sababu tunaiamini imani yetu kuliko Mungu?

### Udhaifu wa kuhakikisha kwetu

Somo la Yn 20:24-29 hutumika mara nyingi kwa mahubiri ya sikukuu ya Jumatatu ya Pasaka. Latukumbusha kwamba mashaka ya kiimani hutokea miongoni mwa Wakristo.

Huonesha pia kwamba hata kama tukitafuta kutiana moyo kwa namna nzuri zaidi kuliko kuambiana tu ni lazima kuamini, bado uhakikisho wetu una mpaka.

Wanafunzi walishindwa kumsaidia Tomaso. Hata walipofanya vizuri kutoa ushuhuda wao, *Tumemwona Bwana*, bado Tomaso aliendelea kushikwa na wasiwasi.

Akina Tomaso bado wapo miongoni mwetu. Tuwasaidieje? Hebu tuangalie zaidi wasiwasi wa Tomaso ulikuwa wa aina gani.

### Uhakiki au uhakika?

Tomaso hutajwa kama mfano hasa wa mtu mwenye kukosa imani. Ndiye picha ya mwenye mashaka.

Lakini je, tumeelewa kweli hali yake na sababu yake ya kutosema tu, Naamini, wanafunzi wenzake walipomwambia kwamba wamemwona Yesu Mfufuka?

Kuna mashaka yanayotokana na mtu kutaka kufanya *uhakiki*. Anapenda kutathmini na kutoa maoni juu ya wengine wanavyomwambia na kumshuhudia, na kila wakati kuna jambo ambalo ana wasiwasi nalo.

Kwa kweli, kinachompa tashwishi ni habari ya kufufuka kwa Yesu. Maana kama hiyo ni kweli, basi lazima aache maisha anayoishi sasa na kumfuata Yesu aendako. Yaani, kimsingi mtu huyo *hataki* kuamini.

Uhakiki hutia shaka kama jambo fulani, k.m. kufufuka kwa Yesu, limetukia kweli. Tomaso hakuwa mtu wa aina hiyo. Alitafuta *uhakika* ambao hutokea mtu anapoondolewa mashaka yake juu ya ukweli wa jambo hilo.

### Tomaso mwenye imani

Tomaso alimwamini Yesu na kutaka kuwa naye akiendelea kumfuata kama alivyofanya miaka mitatu. Lakini Yesu hakuwepo tena kwa Tomaso kama alivyozoea na kupenda. Alishikwa na hofu, lakini si kwa sababu aliangalia imani yake na kuona wasiwasi nayo.

Kilichosababisha kukosekana kwa utulivu wa moyo wake ni kwamba *Yesu* alikosekana. Hiyo inaonekana wazi mara Tomaso anapokutana na Yesu.

Angalia kwanza kwamba Tomaso alibaki kuungana na wanafunzi wa Yesu. Huonesha alitafuta uhakika kwa moyo wote.

Halafu angalia Tomaso anavyomkiri Yesu. Hakuhitaji kufanya uhakiki kuhusu kovu na ubavu wa Yesu. Kuwa pamoja na Yesu aliye hai kulimtosha kukiri, *Bwana wangu na Mungu wangu*.

### Sababu ya kifo cha wasiwasi

Sasa huenda hoja fulani hujitokeza: Tomaso alipata kumwona Yesu kwa macho. Je, si kile kilichomsaidia kusadiki? Vipi na sisi tunaotiliwa wasiwasi siku hizi ila tusiweze kumwona Yesu Mfufuka namna hiyo?

Kama wahubiri wa Neno la Mungu lazima tukubali kwamba maneno yetu mengi kuhusu ulazima wa imani hayasaidii kuamini kweli. Uhakika uliotokana na nguvu ya maneno ya mhubiri hutoweka kesho yake.

Kinachoweza kuua jito la Wasiwasi ni upanga wa Neno la Mungu. Ni habari hizo njema juu ya Kristo Yesu ambazo Yohana (taz. m.30-31) na waandishi wengine walikusanya na kuweka katika Biblia (zingatia k.m. Lk 1:1-4; 1 Pet 1:21.23; 2 Tim 3:14-17).

Kwa njia ya kusikia Injili, wenye mashaka wanaendelea kukutana na Yesu Mfufuka na kutiwa uhakika wa imani kwamba Yesu ndiye Bwana wao na Mungu wao.

*Mch. Philip Bach-Svendsen*

### Mpangilio wa mahubiri

**Utangulizi:**
Kuwasaidia wasikilizaji kukubali kwamba pamoja na kuamini, hutokea tunaona shaka. Tunapoteza nini kama tukikataa wasiwasi huo tulio nao? Jibu: Msaada na uhakika wa kweli hukosekana!

**Mada kuu:**

*1. Tomaso - mwenye imani au wasiwasi?*
- Kufafanua hali ya Tomaso baada ya kifo cha Yesu. Yn 11:16 na 14:5 inaweza kutajwa ili kupanua picha.
- Tomaso kama mtu anayehangaika kushindania imani aliyo nayo.

*2. Tunasaidiaje waaminio wenye wasiwasi?*
- Kosa la kuwaelekeza kwenye imani.
- Msaada wa kumshuhudia Yesu – na mpaka wa msaada huo.
- Kuhakikisha kuwa wenye mashaka wanaendelea kujiunga na usharika na ibada zake.

*3. Yesu Mfufuka anavyomwua jito liitwalo Wasiwasi*
- Kufafanua Yesu alivyomsaidia Tomaso. - Vipi na sisi ambao hatumwoni Yesu kwa macho? Jibu la Yesu katika m.29, na anavyolieleza Yohana katika m.30-31.

**Hitimisho:**
Yesu, Bwana wangu na Mungu wangu! Kumshuhudia Yesu Mfufuka na kumshangilia kwa jinsi anavyowasaidia wenye wasiwasi.

# Uamuzi wangu muhimu na wa busara

Hapo kwanza mimi sikuwa Mkristo. Katika ukoo wetu wote Mkristo alikuwa mmoja tu ambaye ni shemeji yangu, mke wa kaka yangu mkubwa. Japo mama huyu alikuwa Mkristo, lakini mume wake ambaye ni kaka yangu, na watoto wake wawili walikuwa si Wakristo.

Kwa sehemu kubwa tuliamini katika dini za asili za kuabudu miungu isiyojulikana. Baba yangu alikuwa mtu wa kushika sana mila na desturi za kipare. Kila baada ya miaka kadhaa tulikuwa na ibada kubwa ya miungu ambayo kwa jina la kipare iliitwa *Kirurumo*. Hizi zilikuwa ibada za matambiko, na ziliendeshwa na kuhudhuriwa na wanaukoo wote. Tena ziliambatana na kuchinja ng´ombe na kupika vyakula. Na katika sherehe hizi ziliambatana na ngoma na kucheza.

> “Nimekuwa Mkristo kwa miaka mingi, na sijawahi kujuta kwa nini nimekuwa Mkristo.”

Moja ya mambo yaliyokuwa yananishangaza ni namna ambavyo kiongozi wa ibada hizi za mila alikuwa akifanya. Kwanza, ng’ombe aliyetumika kwenye tambiko aliandaliwa maalumu tangu akiwa ndama mdogo. Siku ya tambiko aliwekwa kwenye nyumba maalumu. Kisha, usiku wa manane mzee wa ukoo alimwendea ng’ombe huyu, kumshika sikio na kuanza kumsemesha mambo ya familia, akiamini kuwa kwa njia ya ng’ombe huyu anaongea na mababu waliokwisha kufa.

Wakati hayo yote yanatendeka nilishuhudia jinsi shemeji yangu ambaye ni Mkristo alivyojitenga na mambo haya. Kila mara kaka alipomwuliza kwa nini hashiriki, yeye alijibu kuwa ni Mkristo na anaamini katika Mungu wa kweli ambaye ni Bwana na Mwokozi wa maisha yake. Na kushiriki mambo hayo ni machukizo kwa Mungu wake. Cha ajabu sijawahi kumwona kaka yangu akimgombeza mkewe kwa nini hashiriki, bali mara zote alisema kila mmoja ana uhuru wa kuamini anachoamini.

Ujasiri wa mama huyu ulisababisha nianze kumfuatilia nijue zaidi kuhusu anachoamini. Niligundua hazina kubwa iliyokuwa kwa Mungu wa shemeji yangu. Taratibu nilianza kufuatilia kwa karibu, na hatimaye baada ya muda niliamua kumfuata. Niliamua kubatizwa na kuwa Mkristo.

Kuanzia hapo Kristo akawa ndiye mtawala wa maisha yangu. Tendo hili la imani lilifungua milango ya ukoo wetu, kwani baada ya mimi kuungana na mke wa kaka yangu kuwa Wakristo, watoto wetu wa kwanza na wote waliofuata walibatizwa na kuwa Wakristo. Hata na kaka yangu alibatizwa na kuwa Mkristo akiwa na umri wa miaka 82.

Nimekuwa Mkristo kwa miaka mingi, na sijawahi kujuta kwa nini nimekuwa Mkristo. Sisemi sijakutana na changamoto au magumu baada ya kuwa Mkristo, la hasha. Nimekutana na mambo magumu sana ya kukatisha tamaa, lakini kila nilipopata mambo ya jinsi hiyo, nilimwendea mtawala wa maisha yangu ambaye ni Mungu na kumwomba anisaidie kunivusha.

Mimi sasa ni mzee wa miaka 95, na katika uzee wangu nimepitia mengi na nimeona mengi. Pia nimefanya maamuzi mengi, mengine maamuzi ya busara na pengine wakati mwingine maamuzi ya hovyo. Hata hivyo, uamuzi wangu ambao nauona wa muhimu na wa busara sana ni huu wa mimi kuwa Mkristo. Yeye amekuwa ndani yangu na amenifanya niwe hai. Ameniongoza tangu nilipostaafu kazi mwaka 1987 hadi leo hii ninaposimulia ushuhuda wangu.

Japo sasa naona mwili unadhoofika na wakati wangu wa kuishi hapa duniani unabakia mchache, hata hivyo sina woga wa kufa. Ninasubiri tu siku ikifika nikakae na Mwokozi wangu katika uzima wa milele. Maana najua kwa hakika kuishi kwangu ni Kristo, na kufa ni faida. Hivyo sina woga wala hofu, najua niendako na Bwana wangu ananisubiri. Hata akija mchana au usiku wa manane niko tayari.

*James Sabuni*

*Mahojiano ya ushuhuda huu yalifanyika tarehe 3 Disemba 2023. Majuma mawili baadaye, yaani tarehe 18 Disemba 2023, mzee Gabriel Kadama alitwaliwa na kuzikwa kijiji kwake Lwandai, Soni Lushoto. Sifa, heshima na utukufu ni kwa Mungu wetu aliyetujalia kupata ushuhuda huu kama maneno ya mwisho ya mzee Kadama. Namna alivyotembea na Kristo toka Upagani hadi Ukristo ituimarishe sisi ambao tungali safarini hapa duniani. Sifa, heshima na utukufu zina Mungu wetu.*



*Mzee Gabriel Kadama*

# Kuna maisha baada ya haya!



*Mtu akifa, je! Atakuwa hai tena? Wengi wameuliza kama Ayubu (Ayu 14:14).*

Hisia ya upweke hupita ndani yetu pale tunapoangalia na kutafakari mwisho wa uhai wa mtu. Sisi sote kwa wakati fulani, labda baada ya kifo cha mmoja wa wapendwa wetu, tumejisikia kana kwamba tumbo liko tupu. Hali hii huwa inakuwa na hisia kali, hasa pale mwili wa mpendwa wetu unaposhushwa kaburini kuashiria kuwa huu ndio mwisho wa historia ya uhai wa mtu huyo hapa duniani.

Swali la Ayubu kuhusu jambo hili la maana sana hufuatana na swali lingine: Ni wapi tunaweza kujifunza habari za kile kinachotokea pale mtu anapokufa?

Yesu anatoa ujumbe tunaoweza kuamini. Sababu moja ya utume wa Yesu hapa duniani ilikuwa ni *awaache huru wale ambao kwamba maisha yao yote kwa hofu ya mauti walikuwa katika hali ya utumwa* (Ebr 2:15).

Ni ujumbe wenye faraja. Lakini Yesu ana neno kali pia, akijibu maswali yetu yote juu ya mauti na yale ya maisha ya baadaye kwa uwazi kabisa.

### Uumbaji unatufundisha nini?

Ili kuelewa zaidi kuhusu kifo, turudi kuangalia mwanzo wa uhai wa mwanadamu. Biblia inasema, *Bwana Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi, akampulizia puani pumzi ya uhai; mtu akawa nafsi hai* (Mwa 2:7).

Angalia mtiririko wa habari. Mungu alikuwa amekwisha kumfinyanga Adamu kutoka katika mavumbi ya ardhi. Tayari Adamu alikuwa na umbo zuri ambalo Mungu alipendezwa nalo. Lakini bado hali hii haikumfanya mtu huyu kuwa hai hadi pale Mungu alipompulizia pumzi ya uhai.

Ni hapo uhai ulipoingia ndani ya Adamu kutoka kwa Mungu. Muunganiko huo wa mwili na pumzi ya uhai ulimfanya Adamu kuwa nafsi hai. Mavumbi ya ardhi, jumlisha pumzi ya uhai, tokeo lake ni kiumbe *hai*. Mwili usio na uhai, jumlisha pumzi kutoka kwa Mungu, anapatikana mwenye *nafsi hai*. Kwa kadri tunavyoendelea kuvuta pumzi, tutaendelea kuwa kiumbe hai na nafsi hai mwenye mwili, akili na roho.

### Mtu akifa, nini kinatokea?

Kifo cha mtu ni kinyume cha huo muunganyiko tuliouona katika Mwanzo 2:7. Hutokea utengano. Mtu ambaye alikuwa hai, mwili wake hurudi katika mavumbi ya ardhi ulikotoka na roho yake humrudia Mungu. Mhubiri anasema juu ya *mavumbi kuirudia nchi kama yalivyokuwa, nayo roho kumrudia Mungu aliyeitoa* (Mhu 12:7).

Ni wazi kuwa mtu anapokufa, mwili wake hugeuka kuwa mavumbi. Sisi sote tumeshuhudia. Lakini kwamba roho yake hurudi kwa Mungu hatuoni kwa macho. Huenda tunajiuliza, Je, ni kweli? Na kama roho ikimrudia Mungu inaenda kukaa wapi?

### Lazaro wawili

Yesu alipopata habari ya kifo cha rafiki yake, Lazaro wa Bethania, aliwaambia wanafunzi wake kuwa Lazaro amelala tu, ... *lakini ninakwenda nipate kumwamsha* (Yn 11:11-14). Ndivyo tunavyoamini kuhusu kifo cha wale waliompokea Yesu kama Bwana na mwokozi wa maisha yao. *Wamelala* mauti huku wakingoja Mungu atawaamsha tena. Kwao kifo ni kama usingizi tu. Ni njia ya kuelekea uzima wa milele.

Katika Lk 16:19-31 Yesu anatuambia habari ya Lazaro mwingine. Baada ya kufa, huyo yuko "*kifuani mwake Ibrahimu*" ambapo anafarijiwa baada ya maisha magumu hapa duniani. Ni neno la mfano linalotaka kutuambia kwamba Lazaro amekusanyika pamoja na watu wa imani. Yupo nao "*peponi*", kama Yesu alivyomwambia yule mhalifu (Lk 23:43).


Lakini yupo mwingine pia katika habari hizo. Ni yule tajiri aliyeishi bila kumjali Mungu na amri zake. Anapokufa anajikuta "*kule kuzimu ... alipokuwa katika mateso*". Yesu anaongeza kwamba kati ya Lazaro na huyo tajiri "*kumewekwa shimo kubwa, ili wale watakao kutoka huku [aliko tajiri] kwenda [aliko Lazaro] wasiweze"*.

Yaani, baada ya kifo cha kimwili kuna mahali pawili tofauti sana, na kile kitakachoamua tutakwenda wapi ni jinsi tulivyoamini na kuishi tukiwa hapa duniani. Baadaye hakuna kubadilisha mahali.

### Jibu la kifo cha Yesu

Tunapotafakari juu ya kifo, tunaweza kupata ukweli kamili kupitia kifo cha Yesu Kristo. "*Alizichukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya mti*", akafa, "*ili ... tuwe hai kwa mambo ya haki"* aliyoleta Yesu kwa namna hiyo (1 Pet 2:24). Yesu hakutoweka tu alipokufa, bali alifufuka siku ya tatu, na sasa yuko kama mshindi mkono wa kuume wa Mungu.

Ukweli huu huwapa waamini uhakika kuwa baada ya maisha ya hapa duniani watakwenda kukaa pamoja na Yesu milele.



## Yote yatakuwa mapya

Kama tulivyoona kuhusu kuumbwa kwa mwanadamu, sura mbili za *kwanza* za Biblia husimulia uumbaji wa Mungu wa maskani ya wanadamu iliyokuwa kamili. Sura mbili za *mwisho* za Biblia pia husimulia uumbaji mkamilifu wa maskani ya wanadamu.

Huu ni uumbaji mpya, baada ya ule wa awali kuharibiwa na dhambi. Mara zote Biblia hutuambia kuwa maskani ya milele ya watakatifu ni mahali halisi. Kama vile Yesu alivyofufuka kimwili, ataubadili mwili wa unyonge wa wanaomwamini, upate kufanana na mwili wake wa utukufu, kwa uweza ule aliopewa baada ya kufufuka kwake.

Kwa uweza huo Yesu atavitiisha hata vitu vyote viwe chini yake (Flp 3:21). Kwa hiyo Yohana anaeleza katika kitabu cha Ufunuo juu ya mbingu mpya na nchi mpya, kama vile kutakuwa na Yerusalemu mpya.

Mji huu mtakatifu wa Mungu unaelezwa kuwa hauna vilio wala maumivu, tena maombolezo hayatakuwepo tena. Njia pekee ya kuingia ndani yake ni Yesu (Mdo 4:12). Ni mji ambao wale waliokombolewa kwa damu ya Yesu watakaa daima pamoja na Bwana wao mpendwa. Kama wamwaminio Yesu wa-livyo pamoja naye sasa, na wanapokufa, watakuwa pamoja naye hata milele.





## Ikoje na waliomkataa Yesu?

Mungu ameweka siku atakayowahukumu watu wote kwa haki, kwa mtu yule aliyemchagua. Mtu huyu ni Yesu aliyefufuka katika wafu (Mdo 17:31). *Sisi sote tutasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, ili kila mmoja apate kulipwa kwa ajili ya yale ambayo yametendwa katika mwili wake, yakiwa mema au mabaya* (2 Kor 5:10).

Haijalishi kama tuko hai Yesu akija au tutakuwa makaburini. Yesu anasema kwamba pia wote waliokufa wataisikia sauti yake. *Nao watatoka; wale waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima, na wale waliotenda mabaya kwa ufufuo wa hukumu* (Yn 5:29).

Yesu anaeleza pia hayo matendo anayozungumzia ni matendo ya aina gani. Katika mfano wake kuhusu atakavyowatenga wote katika makundi hayo mawili, matendo yote anayotaja ni yale yaliyotendewa au kutotendewa juu ya "*ndugu zake*". Yaani, Yesu atatumia matendo ya imani katika yeye mwenyewe kama kigezo au kipimo.

Hiyo ni sababu kwa nini wengine watapata hukumu kali: Wamemkataa Yesu. Hali yao hiyo ya kutokuwa na uhusiano naye walipoishi hapa duniani, itaendelea hata baada ya kufa na kupitia kiti cha hukumu cha Kristo. Watasikia Yesu akiwaambia, *Ondokeni kwangu, mlio-laaniwa, mwende katika moto wa milele, aliowekewa tayari Ibilisi na malaika zake* (Mt 25:41).

## Mwenye neno la mwisho

Hukumu hiyo siyo kama Mungu alivyokusudia tangu milele. Mahali hapo pa hukumu alipaandaa kwa ajili ya Shetani tu. Lakini kila anayechagua uongo badala ya ukweli atashiriki hukumu yake aliye baba wa uongo.


Kwa hiyo, kama Yesu anavyotuonya, *afadhali mwogopeni yule awezaye kuangamiza mwili na roho pia katika jehanum* (Mt 10:28). Huyu ndiye pia yule awezaye *kuwaokoa kabisa wao wamjiao Mungu kwa yeye; maana yu hai sikuzote ili awaombee* (Ebr 7:25).

*Christian & James Sabuni*

# Soma Biblia inapendekeza

**Je, unapenda kusoma na kutafakari Biblia? Ila unakosa mwongozo mzuri?**

**Tazama kitabu hiki kipya!**




**Biblia ni hazina isiyoisha kwa imani na maisha yetu yote!**

Kitabu hiki kimeandaliwa kwa mtazamo huu. Kinamwongoza msomaji kusoma *Injili kama alivyoiandika Mathayo Mtakatifu* mtengo kwa mtengo kwa njia hizi nne:

- ***Maelezo*** - hutoa ufafanuzi wa Neno
- ***Fundisho*** - hujumlisha ujumbe wa msingi wa Neno
- ***Maswali*** - humpa msomaji kujihakikishia kuwa ameelewa Neno,
- ***Tafakuri*** - hulenga Neno la Mungu libadilishe maisha ya msomaji ili afanane siku hadi siku na Yesu Kristo

Kurasa 272
Masomo 122

**SOMA BIBLIA**
0759 544 917
S.L.P. 2696, Arusha
editor.somabiblia@gmail.com
www.somabiblia.or.tz

somabiblia

Soma RIZIKI "online"
www.issuu.com/riziki